# JARIDA LA ACT

**TOLEO NA. 42**| JANUARI – MACHI 2022

**Tunaunganisha, Shawishi na Kutetea**

ACT
Agricultural Council of Tanzania

## Wajumbe wa Bodi

Dkt. Jacqueline Mkindi- M/kiti
Mhe. Jitu Soni- Makamu M/kiti
Dkt. Sinare Y. Sinare -Mjumbe
Bw. Fabian Mwkatuma- Mjumbe
Bw. Enock Ndodole- Mjumbe
Bw. Zubery Mwachulla –Mjumbe
Bw. Omary Mwaimu – Mjumbe
Bw. Joeseph Masimba- Mjumbe
Bibi. Elde Kimaro- Mjumbe
Bw.. Abel Lyimo-Mjumbe

## Yaliyomo:

Maonesho ya Biashara ya Dubai

Mafanikio ya Dubai Expo

Mkutano wa Tisa wa Kamati ya Taifa

Mafunzo ya Sera za Biashara

EAFF Yaanda Warsha ya Mwaka

Habari Njema kwa Wafanyabiashra Wa Kati na Wadogo

Mkutano wa NARA

## MAONESHO YA KIMATIFA YA KIBIASHARA (DUBAI EXPO 2020)





# MAONESHO YA KIBIASHARA YA KIMATAIFA - DUBAI EXPO 2020

Maonesho ya Kimatifa ya Kibiashara nchini Dubai maarufu kama Dubai Expo 2020, yalianza tarehe 1 Oktoba 2021 mpaka Machi 31, 2022. Dubai Expo ni jukwaa na tamasha kwa ajili ya watu kutoka mataifa mbalimbali ambapo hukutana kwa pamoja kwa lengo kujifunza sanaa, tamaduni, jiografia, sayansi na teknolojia, ubunifu na vumbuzi mbalimbali; Dubai Expo ilihusisha mataifa 192 Tanzania ikiwemo. Maonyesho ya Dubai yalipambwa kwa mtiriko wa matukio kama vile; siku ya mazao ya asili, siku ya mazao ya mboga mboga na matunda, siku ya misitu ns maliasili, siku ya kongamano la biashara na siku ya kitaifa. Maadhimisho ya Siku ya Tanzania (National Day) yalifanyika Februari 26 2022 na mgeni rasmi alikuwa rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan na kuhudhuriwa na zaidi ya wafanyabiashara 400 kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

ACT iliwakilishwa na Mwenyekiti Dk. Jacqueline Mkindi ambaye alishiriki katika Kongamano Kuu la Biashara lililopambwa na kaulimbiu isemayo ***"Tanzania iko Tayari Kushirikiana na Mataifa Mengine"*** lililofanyika tarehe 27 Machi 2022 kwenye Ukumbi wa Jumeira Beach Resort, Dubai UAE. Tanzania imetumia maonesho ya Dubai kujitangaza katika sekta za utalii, kilimo, mafuta na gesi, madini, nishati, mifugo na uvuvi, ujenzi, usafirishaji pamoja na kutangaza lugha ya ki-Swahili. Kwa kifupi, jumla ya hati 36 za makubaliano (MoUs) zenye thamani ya dola bilioni 7.49 (karibu Sh17.3 trilioni) zilizosainiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na makampuni kutoka Falme za Kiarabu (UAE).



Rais Samia Suluhu Hassan akihutubia hadhara katika Siku ya Tanzania kwenye maonesho ya Dubai

# MAFANIKIO YA MAONESHO YA KIMATAIFA YA KIBIASHARA (DUBAI EXPO 2020)

Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe (Mb) alisaini hati za makubaliano (MoUs) na makampuni ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE). Mikataba hiyo imelenga kukuza na kuongeza ustawi wa sekta ya kilimo nchini. Kampuni zilizoingia mikataba ni; - Ofisi Binafsi ya Mtukufu Sheikh Ahmed Dalmook Al Maktoum, AFRIDE, DMCC, na Agritech Global.



Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe (Kulia) akisaini hati za makubaliano katika maonesho ya Dubai 2020

Mkurugenzi Mtendaji wa TAHA, Dk. Jacqueline Mkindi alisaini hati ya makubaliano (MoU) na MV AGRO FRESH kutoka India kwa lengo la kufungua milango ya kibiashara hususani mazao ya mboga mboga na mtunda.



Katika picha: Mkurugenzi Mtandaji wa TAHA, Dkt. Jacqueline Mkindi (Kulia) akisaini hati ya makubaliano

Makubaliano 36 yalitiwa saini na Serikali ya Jamhuri wa Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) katika Kongamano la Biashara na Uwekezaji Tanzania. Mikataba hiyo inahusisha uwekezaji katika sekta za nishati, kilimo, utalii, miundombinu, usafirishaji, nguo, TEHAMA na sekta nyinginezo nchini. Mikataba iliyosainiwa inakadiriwa kutengeneza ajira takribani 204,575 kwa raia na wasio raia wa Tanzania.

# MKUTANO WA TISA WA KAMATI YA KITAIFA

Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji iliandaa Mkutano wa Tisa (9) wa Kamati ya Kitaifa inayoshughulikia Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula (National Sanitary and Phytosanitary Measures Committee - NSPSC). Mkutano huo ulifanyika kuanzia tarehe 16 hadi 18 Februari 2022 katika Hoteli Nashera, Mkoani Morogoro na uliandaliwa kwa ufadhili wa Shirika la *Trade Mark East Africa* (TMEA). Kikao kiliongozwa na Bw. Lazaro H. Msasalaga - Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora, kutoka Shirika la Viwango Tanzania. (TBS); lengo kuu la Mkutano huo, ilikuwa ni kujadili utekelezaji wa shughuli za Kamati ya Kitaifa ya kushughulikia Vigezo vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula.  ACT iliwakilishwa na Bw. Khalid Ngassa, Meneja Huduma kwa Wanachama ambaye alitoa wasilisho la utekelezaji wa shughuli zilizotekelezwa na ACT zinazohusiana na afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula. TMEA inatekeleza mradi wa miaka mitatu nchini, ambao umeanza Julai 2021 mpaka Julai 2024, na umelenga zaidi Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula.

TMEA ilianzishwa mwaka 2010 ili kukuza ustawi wa biashara ukanda wa Afrika Mashariki. TMEA inafanya kazi kwa karibu na mashirika ya kikanda ya kiserikali, ikiwa ni pamoja na Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Mamlaka ya Maendeleo ya Kiserikali (IGAD), Soko la Pamoja la Afrika Mashariki na Kusini (COMESA), Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), serikali za kitaifa, sekta binafsi, na mashirika ya kiraia.



Wanakamati wakiwa kwenye picha ya pamoja

# MAFUNZO JUU YA SERA ZA BIASHARA


Shirikisho la Vyama vya Wakulima Kusini mwa Afrika (SACAU) kwa kushirikiana na taasisi ya AHA kutoka nchini Ujerumani waliandaa mafunzo ya siku tatu kuhusu *"**Uwezo wa Mashirika ya Wakulima kusimamia Biashara za Kikanda**"* yaliyofanyika kuanzia tarehe 13 hadi 16 Machi 2022, katika Hoteli ya New Centurion mjini Johannesburg, Africa Kusini. Lengo kuu la mafunzo hayo lilikuwa ni kuangazia nafasi ya Mashirika ya Wakulima katika udhibiti wa ubora wa Afya ya Wanyama na Usalama wa Chakula kwenye mnyororo wa thamani wa kuku. Bi. Belinda S. Kancheya kutoka Shirika la Viwango la Zimbabwe (ZBS) na Mratibu wa Kitaifa wa SADCSTAN alifanya wasilisho kuhusu viwango vya SADC vinavyosimamia mnyororo wa thamani wa kuku kikanda.

Kwa kifupi, ukanda wa SADC, tuna changamoto katika upatikanaji wa taarifa na tafiti zinazohusu mnyororo wa thamani wa kuku; kuna haja ya kuanzisha jukwaa la kikanda ambalo litaunganisha wajasiriamali wa kuku kwa lengo la kutanua wigo wa masoko na kubadilishana uzoefu. SACAU imeahidi kuharakisha uanzishwaji wa jukwaa hilo kwa wajasiriamali wa kuku. ACT iliwakilishwa na Bibi. Elde Kimaro (Mjumbe wa Bodi ya ACT), Bi. Avelina Bernard, Bw.Obedi Abraham na Bw. Khalid Ngassa kutoka Sekretarieti ya ACT.

# EAFF YAANDAA WARSHA YA MWAKA

Shirikisho la Wakulima wa Afrika Mashariki (EAFF) liliandaa warsha ya siku mbili kuanzia tarehe 1 hadi 3 Februari 2022 iliyofanyika katika Hoteli ya Ramada Resort, Dar es Salaam-Tanzania. Warsha hiyo ya kila mwaka, ilihudhuriwa na washiriki 50 ambao walitoka nchi 13 wanachama. EAFF imepokea ruzuku kutoka Umoja wa Ualaya (EU), IFAD, na Shirika la Afrika, Caribbean, na Pacific kutekeleza mradi unaofahamika kwa jina la "Mashirika kwa Nchi za Afrika, Karibea na Pasifiki (FOA4CP)". Baraza la Kilimo Tanzania (ACT) liliwakilishwa na Bw. Omary Mwaimu (ACT na Mjumbe wa Bodi ya EAFF) ambaye aliwasilisha taarifa ya utekelezaji kitaifa. Mradi wa FOA4CP unalenga wakulima wadogo wanaojihusisha mazao kama; mihogo, maziwa, viazi vya lishe, mahindi na soya katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Shirikisho la Wakulima wa Afrika Mashariki (EAFF) ni muungano wa mashirikisho 24 ya kitaifa ya wakulima, mashirika ya kitaifa ya ushirika, na vyama vya kitaifa vya bidhaa za kilimo kutoka nchi kumi (10) za Afrika Mashariki;-Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Djibouti, Eritrea, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Sudan Kusini, Tanzania, na Uganda.




Bw. Omary Mwaimu (Mjumbe wa Bodi ya ACT na EAFF) akitoa neno la ufunguzi wa warsha

# HABARI NJEMA KWA WAFANYABIASHARA WADOGO WA WA KATI

Baraza la Kilimo Tanzania (ACT) imesaini hati ya makubaliano kwa kipindi cha miaka miwili (MoU) na Taasisi ya Kimataifa "***Aceli Africa"*** kwa lengo la kuwajengea uwezo wafanyabiashara wadogo na wakati katika sekta ya kilimo ili waweze kutumia fursa za kupata mitaji ya kuendesha shughuli zao. ACT na Aceli Africa zitatekeleza majukumu yafuatayo;-

i. Kuhamasisha wadau katika mfumo ikolojia wa fedha za kilimo, kuchambua na kukutana na wadau watakaosaidia kuweka mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara wadogo na wakati
ii. Kuwajengea uwezo wafanyabiashara wadogo na wakati ili wakidhi vigezo vya kupata mitaji
iii. Kuchambua changamoto za kisera zinazowakabili wafanyabiashara wa dogo wa wakati kwa kushirikiana na Serikali na wadau mbalimbali.

# MKUTANO WA KUKAMILISHA ANDIKO LA AGENDA ZA KILIMO (NARA)

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) iliandaa mkutano wa kukamilisha andiko la NARA uliofanyika Dodoma katika majengo ya uwanja wa ndege. ACT ilishriki katika mkutano huo wa siku moja ya tarehe 10 Machi 2022 uliyolenga kupokea maoni ya wadau kuhusu Agenda ya Kitaifa ya Utafiti kwenye Kilimo (NARA) kwa kipindi cha miaka mitano ijayo kuanzia 2022. ACT ilikuwa sehemu ya kikosi kazi kilichotengeneza Agenda hiyo na iliwakilishwa na Susan Masagasi kutoka Mradi wa PFS na ambaye pia aliwakilisha ACT kwenye mkutano huo. Agenda hii imeandaliwa kwa madhumuni ya kutoa mwongozo katika tafiti za kilimo ili kuhakikisha kuwa matokeo ya tafiti hizo zinanufaisha taifa kiuchumi na kuboresha maisha ya watu. Kwa sasa Agenda hii imefikia mwisho tayari kwa kusainiwa na viongozi wa Wizara ya Kilimo.

## Tukio Lijalo

## Weka Alama kwenye Kalenda Yako

1. Maonesho ya Kilimo (Agri Expo 2022) yatafanyika Aprili 13 na 14 kwa njia ya mtandao. Tembela [www.africa-agriexpo.com](http://www.africa-agriexpo.com)

2. Maonesho ya Nane Nane

**Tunaunganisha, Shawishi na Kutetea**

## Dira na Dhamira ya ACT

**DIRA**

Kuwa na Sekta ya Kilimo iliyofanikiwa, endelevu na shindani: inayohakikisha usalama wa chakula na lishe unaotokana na msukumo wa kisekta binafsi
.

**DHAMIRA**

Kutetea, kuratibu na kuwezesha mazingira rafiki kwa kilimo-biashara

## Malengo ya ACT

- Kujenga mazingira wezeshi kwa kilimo-biashara
- Kujengea uwezo wanachama wa ACT katika utoaji wa huduma
- Kutuma na kupokea taarifa kutoka wanachama na wadau wengine zinazohusu ustaw wa Sekta ya Kilimo nchini.
- Kuratibu na kuendesha mashirikiano katika ngazi ya taifa na wilaya
- Kuratibu jitihada za Sekta ya Umma na Binafsi katika uendelezaji wa Kilimo biashara


## *Bodi ya Uhariri*

1. ***Mr. Timoth Mmbaga - Mwenyekiti***
2. ***Mr. Mark Magila- Mjumbe***
3. ***Ms. Laetitia William - Mjumbe***
4. ***Mr. Khalid Ngassa- Mjumbe***
5. ***Mrs. Susan Masagasi- Mjumbe***



## Wasiliana Na.

Mkurugenzi Mtendaji
Agricultural Council of Tanzania
S.L.P 14130,
Dar es
Salaam.

**Simu:** +255 22 2761344,
**Nukushi:** +255 22 2128032
**Barua pepe:** act@actanzania.or.tz
**Tovuti:** www.actanzania.or.tz


# Hii ndiyo PFS

***Ubia wa Mradi wa PFS"*** unaratibu na kuwezesha watendaji mbalimbali kwenye mnyororo wa thamani wa wadau chini ya mfumo wa mashirikiano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP). Mradi unatekelezwa na Baraza la Kilimo Tanzania (ACT). Lengo lake ni kuchangia na kuongeza kiwango cha mafanikio yaliyopatikana kwenye awamu ya pili ya Mradi wa Ubia wa Kilimo Tanzania (TAP II) katika kipindi cha Oktoba 2014 had Mei 2020. Mradi huo ulifanikiwa ukuaji wa kilimo kwa kutumia mbinu za kilimo biashara na uwekezaji.

### Malengo ya Mradi

**Lengo kuu ni;**Kuongeza usalama wa chakula na lishe, na kupunguza umasikini. Umaskini unatarajiwa kupungua kwa 17%, halikadhalika na ukosefu wa lishe kwa watoto kupungua kwa 5%.

### Utaratibu wa Utekelezaji

Mradi utatumia mbinu ya ubia katika utekelezaji wa mradi. Mradi wa PFS, chini ya Baraza la Kilimo Tanzania (ACT) utaratibu na kuongeza uwezeshaji na utekelezaji ili kuhakikisha ubia unaimarishwa na mafanikio tarajiwa yanafikiwa. Mradi unatumia ujuzi na maarifa ili kutatua vikwazo muhimu kwenye mnyororo wa thamani. Mradi umeainisha Asasi za Kiraia 35, wabia kutoka setka ya umma na binafsi (ndani na nje ya nchi), wenye uwezo na majukumu mbalimbali watakaoshirikishwa katika kazi ya ubia


**Kwa taarifa zaidi, wasiliana na:**
Mratibu Taifa
Mradi wa PFS
S.L.P 14130, Dar es Salaam Email:
act@actanzania.or.tz
Tovuti:www.actanzania.or.tz


***PFS inawajibika kwa Bodi ya Wakurugenzi wa ACT***